## 19-Idhwhaar Na Idghaam Katika Laam

**Idhwhaar na Idghaam katika Laam:**

ل (Laam) ya المعرفة (al-ma'rifah- kibainishi) inapokuwa mbele ya herufi za hijaaiyah hugawika katika hali mbili; Herufi za الشَّمْسِيَّة (ash-shamsiyah - jua) na za الْقِمَرِيَّة (al-qamariyah - mwezi). ل hiyo hutamkwa ima kwa idhwhaar au kwa idghaam.

**Idhwhaar katika Laam:**

ل (Laam) ya kibainishi yenye kuingia katika jina hudhihirishwa inapokuwa herufi inayoifuatia ni katika herufi za qamariyyah; ambazo zimekusanyika katika ibara:

أَبْغِ حَجّكَ وَخَفْ عَقِيمَهْ

Herufi za qamariyyah zimeitwa hivyo kwa kuwa huwajibika kudhihirisha ل iliyoko kabla ya hizo herufi kama inavyodhihirishwa katika neno la الْقَمَر (al-Qamar - mwezi) na alama yake ni kuweko sukuwn.

**Idghaam katika Laam:**

ل (Laam) ya kibainishi iliyo saakin huingizwa kwenye herufi inayoifuatia ikiwa herufi hiyo ni katika herufi za shamsiyyah (jua) ambazo ni herufi zote zisizokuwa herufi za qamariyyah (mwezi); nazo zimekusanyika katika kila mwanzo wa neno kwenye ibara:

طِبْ ثُمَّ صِلْ رَحِماً تَفُزْ ضَفْ ذاَ نَعَمْ دَعْ سُوءَ ظَنَّ زُرْ شَرِيفاً لِلكَرَم

Herufi za shamsiyyah: Zimeitwa hivyo kwa kuwa huwajibika kuingiza ndani yake ل iliyoko kabla ya hizo herufi kama inavyoingizwa katika neno الشَّمْس (ash-shams – jua) na alama yake ni kutokuweko sukuwn na kuweko shaddah katika herufi inayofuatia.

| Herufi za shamsiyah<br>Idghaam | | | Herufi za qamariyah<br>Idhwhaar | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Matamshi** | **Neno** | **Herufi** | **Matamshi** | **Neno** | **Herufi** |
| at-twufaan | ٱلطُّوفَانَ | ط | al-Aakhirah | ٱلْأَخِرَةُ | أ ء |
| ath-thamaaraat | ٱلثَّمَرَٰتِ | ث | al-ba'th | ٱلْبَعْثِ | ب |
| as-Swalaah | ٱلصَّلَوٰةَ | ص | al-ghayth | ٱلْغَيْثَ | غ |
| ar-Ra'd | ٱلرَّعْدُ | ر | al-haqq | ٱلْحَقُّ | ح |
| At-Ttawwaab | ٱلتَّوَّابُ | ت | al-Jannah | ٱلْجَنَّةَ | ج |
| adhw-dhwalaalah | ٱلضَّلَٰلَةَ | ض | al-Kawthar | ٱلْكَوْثَرَ | ك |
| adh-dhaakiriyn | ٱلذَّٰكِرِينَ | ذ | al-wuhuwsh | ٱلْوُحُوشُ | و |
| an-nakhl | ٱلنَّخْلِ | ن | al-khayraat | ٱلْخَيْرَٰتِ | خ |
| ad-duniyaa | ٱلدُّنْيَا | د | al-fiyl | ٱلْفِيلِ | ف |
| as-samaaaa | ٱلسَّمَآءِ | س | al-'abd | ٱلْعَبْدُ | ع |
| adhw-dhwulumaat | ٱلظُّلُمَٰتِ | ظ | al-Qiyaamah | ٱلْقِيَٰمَةِ | ق |
| az-zaytuun | ٱلزَّيْتُونِ | ز | al-yawm | ٱلْيَوْمِ | ي |
| ash-sharr | ٱلشَّرَّ | ش | al-Muddath-thir | ٱلْمُدَّثِّرُ | م |
| al-layl | ٱلَّيْلِ | ل | al-Hudaa | ٱلْهُدَىٰ | هـ |